**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SONGEA**
**MTIHANI WA MOKO KATA YA MFARANYAKI 2024**
**SOMO LA HISABATI DARASA LA VII**

**Muda: Saa 2**

**MAELEKEZO**

- ☐ Mtihani huu una sehemu 3 A, B, C
- ☐ Jibu maswali yaote katika sehemu A, B na C
- ☐ Onyesha kazi yako vizuri na kwa mpangilio




**SEHEMU A: MATENDO YA KIHISABATI**

| SWALI | KAZI | JIBU |
|---|---|---|
| 1. i) Tafuta jumla ya 768786 na 96708 | | |
| ii) Ni nini tofauti ya 276876 na 968768 | | |
| iii) Zidisha 6006 na 700 | | |
| iv) Vitabu 84084 viligawiwa katika shule tofauti 84. Je kila shule ilipata jumla ya vitabu vingapi? | | |
| v) Mtoto alipima uzito na kuwa na kilo 20.06, na mama wa mtoto alikuwa na kilo 62.05. Je nini jumla ya uzito wao. | | |
| vi) Wilaya ya Songea ilizalisha tani 5356, za mahindi kwa miaka 5 mfululizo. Je nini jumla ya mahindi yote. | | |
| vii) Mtoto alikula $\frac{1}{4}$ ya chungwa, kisha mama akala $\frac{1}{2}$ ya chungwa lote. Je sehemu gani ya chungwa iliyobaki. | | |
| viii) Wanafunzi wa shule ya msingi Zimanimoto hutumia kilogramu $6\frac{1}{2}$ ya mchele kwa mlo mmoja. je watatumia kilogramu ngapi katika siku tano? | | |
| ix) Mr. Bakari alikuwa na deni la shilingi 300, kisha akalipa shilingi 100. Je alibaki na deni la shilingi ngapi? | | |
| x) Namba $^{-}7$ ikijumlishwa na namba gani jibu litakuwa $^{+}5$ | | |

## SEHEMU B: MAUDHUI YA MAFUMBO (Alama 30)

| | | |
|---|---|---|
| 2. i) Fafanua namba ifuatayo 7408 | | |
| ii) Mwanafunzi alipewa tarakimu 2,0,7,8,4,9 aliambiwa apange namba hizo ili kupata tarakimu kubwa zaidi. Je mpangilio sahihi ni upi? | | |
| iii) Gari hutumia wastani wa lita 1 ya petrol kusafiri umbali wa km 5. Je gari likisafiri umbali wa km 200. Litatumia kiasi gani cha mafuta | | |
| iv) Ikiwa watu 6 hulima shamba lenye ekari 4 kwa siku 3. Je watu 12 watalima shamba hilohilo kwa siku ngapi? | | |
| v) Mzee Machaku alikuwa na shamba la ekari 810. Aliwapatia wanawe watatu Jonh, Halima na Abdallah kwa uwiano wa 1:2:6. Je Abdallah alipata ekari ngapi? | | |
| vi) Miaka mitano mfululizo wanafunzi wa shule ya msingi Misufini walizalisha mazao ya mahindi kama ifuatavyo:- mwaka MCMXC walizalisha kiasi cha kg CC za mahindi, mwaka MM kg CD za mahindi, mwaka MMV kg CDiii, mwaka MMX kg CCCiv za mahindi na mwaka MMXV kg CCL za mahindi. Andika jumla ya mazao ya miaka yote kwa namba za kiarabu. | | |
| 3. i) Je ni namba ipi itafuata katika mfululizo wa namba zifuatazo? 23, 29, 31_____ | | |

| | | |
|---|---|---|
| ii) Katika namba 76827302. Ni nini thamani ya tarakimu 6? | | |
| iii) Joyce alisafiri umbali wa km 200 kutoka Songea hadi Makambako na alitumia saa 5. Je alisafiri kwa mwendokasi gani? | | |
| 4. i) Jua huchomoza saa kumi na moja na nusu alfajiri. Andika saa hiyo katika mtindo wa saa 24. | | |
| ii) Je ni namba gani kubwa inaweza kugawa namba 24, 36 na 72. | | |
| iii) Ana aliambiwa atafute kigawo kidogo cha shirika katika namba 4, 6 na 12. Je jibu sahihi ni lipi? | | |
| 5. i) Juma hupokea mshahara wa shilingi 200,000/= hutumia $\frac{1}{2}$ ya mshahara wake kununua chakula, na $\frac{1}{4}$ ya mshahara wake kununua mavazi. Je hubakiwa na kiasi gani? | | |
| ii) Maktaba ya mkoa ina jumla ya vitabu vifuatavyo vya darasa la saba kwa masomo kama ifuatavyo:- vitabu 40 vya kiada vya Kiswahili, vitabu 30 vya kiada vya sayansi na vitabu 20 vya kiada vya Hisabati. Ikiwa $\frac{1}{4}$ ya vitabu vyote vilipotea. Je kila somo lilibakiwa na vitabu vingapi? | | |
| iii) Umri wa Juma na Ana miaka 10 iliyopita ilikuwa jumla ya miaka 20. Ikiwa umri wa Juma wa sasa ni miaka 22. Je nini jumla ya umri wa Ana wa sasa. | | |
| 6. i) Tafuta thamani ya mlinganyo ufuatao ukiwa kama mtaalamu wa hisabati $(64 \div 8 \times 4) + 34 - 4$ | | |

| | | |
|---|---|---|
| | | |
| ii) Mwajuma aliambiwa aorodheshe namba shufwa zilizopo kati ya 50 na 75. Je Mwajuma aliorodhesha namba zipi? | | |
| iii) Mwalimu alimwambia mwanafunzi afikirie namba kisha ajumlishe na sita na agawanye jumla kwa 2 na jibu apate 20. Je namba hiyo ni ipi? | | |
| **SEHEMU C: MAUMBO NA TAKWIMU (Alama 10)** | | |
| 7. i) Mwalimu wa Hisabati alimtaka Samia kutafuta thamani ya x katika pembetatu ifuatayo:<br><br> | | |
| ii) Debora aliambiwa atafute eneo la umbo lifuatalo<br><br> | | |
| iii) Mwajuma alikula robo tatu ya chungwa lenye nusu kipenyo cha sm 49. Je nini jumla ya eneo la chungwa lote alilokula Mwajuma? | | |
| 8. i) Kielelezo kifuatacho kinaonyesha idadi ya wanyama. Mabadiliko ya hali ya hewa yamepelekea idadi kubwa ya simba kupungua. Tafuta idadi ya simba wote waliobaki katika mbuga ya mikumi ikiwa wanyama wote walikuwa ni 720<br><br> | | |
| ii) Doris alipewa noti nne za shilingi elfu kumi akanunua vitu vifuatavyo: machungwa 30@3 sh. 300, sabuni miche 6@sh.3,000, viatu pea 2@sh. 5,000. Je alibakiwa na shilingi ngapi? | | |